

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA KUMI NA TISA**

**06 MEI, 2024**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**KIKAO CHA KUMI NA TISA – TAREHE 06 MEI, 2024**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha

2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **242. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini mkakati wa Serikali wa kumaliza tatizo la matundu ya vyoo, viti, meza na madawati katika Halmashauri zote nchini.

#### **243. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESHER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini ujenzi wa barabara ya Mhanga hadi Mgeta-Kilolo utaanza.

**244. MHESHIMIWA VENANT DAUD PROTAS (IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Halmashauri ya Wilaya ya Uyui itagawanywa na kutoa Halmashauri mpya ya Kizengi.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**245. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, kwa nini wanufaika wa TASAF wanalazimika kufuata fedha Benki hata fedha hiyo ikiwa ni kidogo.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**246. MHESHIMIWA ZAHOR MOHAMMED HAJI (MWERERA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, nini mpango wa Serikali kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika kuwakinga Wananchi na madhara yanayoweza kutokea.

**247. MHESHIMIWA OMAR ISSA KOMBO (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, lini Serikali itafanyia kazi Changamoto ya Kodi na Tozo kwenye Fedha za Mfuko wa Jimbo kwa upande wa Zanzibar.

**WIZARA YA NISHATI:**

**248. MHESHIMIWA SAMWELI XADAY HHAYUMA (HANANG’):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha kupooza Umeme Hanang’.

**WIZARA YA MAJI:**

**249. MHESHIMIWA HAMISI SHABANI TALETALE (MOROGORO KUSINI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itapeleka maji Kata ya Tununguo katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki.

**250. MHESHIMIWA EDWARD OLELEKAITA KISAU (KITETO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itamaliza tatizo la maji Kiteto.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**251. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMEDI KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, upi mpango wa Serikali wa kuipatia Gari la Zimamoto Wilaya ya Liwale ili kukabiliana na majanga ya moto.

**252. MHESHIMIWA FELISTA DEOGRATIUS NJAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali italeti Bungeni Muswada wa Sheria ya kuboresha Sheria za Jeshi la Magereza ili ziendane na wakati.

**253. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini ujenzi wa Kituo cha Polisi Tarafa ya Igurubi – Igunga utakamilika.

**WIZARA YA AFYA:**

**254. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itajenga jengo la kuhifadhia Maiti katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Katavi.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**255. MHESHIMIWA ABEID IGHONDO RAMADHANI (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukomesha mapenzi ya Jinsia moja nchini pamoja na ukatili dhidi ya Watoto.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **256. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kuna mpango gani kuhakikisha kila Chuo Kikuu na Vyuo Vishiriki vinashirikiana na Halmashauri ili kuwezesha Vyuo hivyo kutekeleza umahiri wao.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**DODOMA**  
**06 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**